

MAANDALIO YA SOMO YA KISWAHILI GREDI YA 6

MUHULA WA 1

WIKI 1

SHUL E	GREDI	ENEO LA KUJIFUNZA	TARE HE	MUD A	MAHUDHUR IO
	GREDI YA 6	KISWAHILI			

WIKI 1: SOMO 1

- **Mada:** VIUNGO VYA MWILI VYA NDANI
- **Mada Ndogo:** Kusikiliza na Kuzungumza (Matamshi Bora: Silabi na Sauti)
- **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa:** Kufikia mwisho wa somo, mwanafunzi aweze kutambua silabi zinazotokana na sauti *d/nd*, *ch/sh*, *j/nj* na *g/ng* katika maneno.
- **Swali Dadisi:** Je, unajua maneno gani yenye silabi za sauti *d/nd*, *ch/sh*, *j/nj* na *g/ng*?
- **Nyenzo:** Kadi za silabi lengwa, vifaa vya kidijitali, Kiswahili Sahili Grd 6.
- **Mpangilio wa Ujifunzaji:**
 - **Utangulizi (Dakika 5):** Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutaja maneno mbalimbali wanayoyajua.

o **Ufanikishaji (Dakika 25):**

- **Hatua 1:** Mwanafunzi atambue silabi za sauti *d/nd, ch/sh, j/nj* na *g/ng* (k.m. doa/ndoa, choka/shoka) ubaoni au kwenye vitabu.
- **Hatua 2:** Mwanafunzi asikilize silabi za sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu au kupitia kifaa cha kidijitali.
- **Hatua 3:** Wanafunzi watamke silabi hizo kwa usahihi ili kuimarisha matamshi.

o **Hitimisho (Dakika 5):** Maswali na majibu kuhusu sauti zilizofunzwa.

- **Shughuli za Ziada:** Kutafuta maneno zaidi yenye sauti lengwa.
- **Tathmini ya Mwalimu:**

SHUL E	GREDI	ENEO LA KUJIFUNZA	TARE HE	MUD A	MAHUDHUR IO
	GREDI YA 6	KISWAHILI			

WIKI 1: SOMO 2

- **Mada:** VIUNGO VYA MWILI VYA NDANI
- **Mada Ndogo:** Matamshi Bora (Vitanzandimi)